HALMASHAURI YA WILAYA KIBAHA

TOVUTI: www.ruvusecondary.sc.tz
SIMU:0786313310**(MKUU WA SHULE**
0716626465**(MAKAMU MKUU WA SHULE)**
0755970137/ 0713943193 (MWL. MALEZI)
0716724562 (MWALIMU TAALUMA)

SHULE YA SEKONDARI RUVU
S.L.P 72
MLANDIZI

TAREHE……

KUMB.NA RSS/MS/189/2021
MWAFUNZI……..
S.L.P……
……

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE KIDATO CHA TANO 2021/22

1.0 **UTANGULIZI**

Ninayo furaha kukutaarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha Tano katika Shule ya Sekondari Ruvu kwa Mwaka wa masomo **2021/2022** Tahasusi (combination) ya …….. Unapaswa kufika Shuleni tarehe……kabla ya saa 11 jioni bila kukosa ukiwa umevaa sare ya Shule.

1.**1 JINSI YA KUFIKA SHULENI:**

Shule ipo Wilaya ya Kibaha Mkoa wa Pwani Km 77 kutoka Dar es salaam kando ya barabara kuu iendayo Morogoro. Ni kati ya Mlandizi na daraja la Mto Ruvu.

2.0 **ADA NA MICHANGO YA SHULE**

NA	MICHANGO	KIASI
1.	**Ada ya Shule**	**Sh. 70,000.00 kwa mwaka**
		Sh. 35,000 .00 kwa muhula
2.	**Taaluma**	**Sh. 20,000.00 kwa mwaka**
3.	**Tahadhari**	**Sh. 5,000.00 haitarejeshwa**
4.	**Ukarabati wa Samani**	**Sh. 15,000.00 mara moja**
5.	**Matibabu(huduma ya kwanza)**	**Sh. 10,000 .00 kwa mwaka**
6.	**Malipo ya vibarua(ulinzi na upishi)**	**Sh. 30,000.00 kwa mwaka**
7.	**Kitambulisho**	**Sh. 5,500.00 mara moja**
8.	**Kukodi godoro**	**Sh. 10,000.00 kwa mwaka**
9.	**Mtihani wa kupijima(Mock)**	**Sh. 20,000.00 kwa mwaka**
10.	**Nembo ya shule**	**Sh. 2500.00**
	JUMLA	**Sh. 188,000.00**

Fedha hizi zilipwe kwenye akaunti ya Shule **NMB A/C Na. 21201200100** Jina la akaunti ni **RUVU GIRLS HIGH SCHOOL**. Mwanafunzi aje na karatasi ya Benki **(BPS**) shuleni siku anayoripoti ikionyesha Jina kamili la Mwanafunzi na tahasusi yake. Hakikisha unabaki na nakala moja ya karatasi ya Benki.

NB: MALIPO YOTE YA SHULE YALIPWE BENKI. HATUPOKEI PESA TASLIMU ZA ADA NA MICHANGO YA SHULE ILIYOORODHESHWA HAPO JUU KATIKA JEDWALI.
KUMBUKA KUANDIKA JINA KAMILI LA MWANAFUNZI

3.0 **MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA**: Tafadhali mzazi tekeleza yafuatayo:

3.1 **SARE YA SHULE**

3.1.1 **Sare ya Darasani ni:**

- Sketi mbili ndefu za rangi ya kijani mkolezo(**Dark green**) zishonwe Marinda boksi (Kitambaa kimeambatanishwa). Ziwe ndefu mpaka kwenye vifundo vya miguu na si vinginevyo
- Mashati meupe (Tomato) ya mikono mifupi mawili(2)
- Soksi ndefu nyeupe jozi mbili au zaidi(Free size)
- Sweta ya kijani mkolezo(Dark green) yenye shingo V
- Aje na tai ya kijani yenye michirizi myeupe iliyokatiza.
- Viatu vyeusi vya kufunika vyenye soli fupi jozi mbili (visiwe na urembo)
- Tisheti ya orange (rangi ya chungwa) yenye nembo ya shule. Ni vema aje kununua maeneo ya jirani na shule ili kupata nembo ya shule.

  NB: Kwa wanaovaa hijabu watashona nusu kanzu nyeupe (badala ya shati) yenye urefu wa kufunika mikono na ifike chini ya makalio. Aidha ushungi (juba) uwe mweupe wenye kufunika mikono usio na urembo wowote.

3.1.2 **Sare ya Kushindia ni:**

- Mwanafunzi ashone gauni ya solo ndefu hadi kwenye vifundo vya miguu. Kitambaa kiwe kizito (sio tetroni) cha rangi ya drafti nyeupe, nyeusi na maruni. Kitambaa kimeambatanishwa.
- Aje na simple shoes(viatu vya wazi)vyenye kisigino kifupi

  NB: Kwa wanaovaa hijabu ya kushindia iwe ya rangi ya maruni(Damu ya mzee) ya kitambaa kizito yenye kufunika mikono na isiwe na urembo.

3.1.3 **Sare ya Michezo ni:**

- Track suit ya rangi ya bluu mkolezo(Dark blue) pamoja na fulana yake (jezi) iwe na mistari mweupe pembeni na isiwe ya kubana.
- Aje na raba nyeupe jozi moja

3.1.4 **Sare ya Maabara:**

- Mwanafunzi anayesoma masomo ya sayansi PCB, PCM, CBA na CBG ashone koti jeupe lenye urefu mpaka chini ya goti kwa ajili ya matumizi wakati wa practical. Aidha kwa anayesoma **Baolojia** awe pia na dissecting kit

3.1.5 **Sare wakati wa kujisomea jioni (Evening Preparation)**

- Mwanafunzi ashone suruali ya kitambaa cheusi kizito na iwe pana(Isiyobana)
- Mwanafunzi aje na fulana / tisheti nyeupe yenye kola maarufu kama form six isiwe na maandishi wala urembo wowote.
- Aje na soksi nyeusi ndefu(free size)

  ZINGATIA Sare za Shule zitavaliwa na mwanafunzi kwa kipindi chote atakachokuwa shuleni kwa kuzingatia ratiba ya masomo, kazi za nje na michezo. Aidha mwanafunzi atavaa sare ya shule atokapo nje ya shule na anaposafiri kwenda likizo na kurudi shuleni. Ni marufuku kuja na mavazi ya nyumbani au kuvaa urembo, kunyoa kipara, kusuka au kufuga nywele, kutumia madawa ya nywele na ya kujichubua, kupaka rangi kucha au midomo. Mwanafunzi hatakiwi kuvaa pete, bangili, hirizi au hereni.

3.**2 MAHITAJI MUHIMU AMBAYO MWANAFUNZI ANAPASWA KULETA SHULENI.**

Mzazi /mlazi anatakiwa kuchangia huduma za elimu kwa ajili ya matumizi binafsi ya mwanafunzi awapo shuleni kama ifuatavyo:

3.2.1 Bunda (Ream) moja ya karatasi aina ya **A4**

3.2.2 Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (orodha imeambatanishwa)

3.2.3 Sanduku la bati (tranka) na kufuli imara, pia begi la madaftari. Masanduku mengine hayaruhusiwi.

3.2.4 Shuka nne za rangi ya pinki pamoja na mto na foronya za pinki

3.2.5 Vibanio vya kuanikia nguo

3.2.6 Chandarua ya kuzuia mbu ya pembe nne rangi nyeupe(isiwe ya duara)

3.2.7 Ndoo ndogo ya kuogea pamoja na vyombo vya chakula (yaani kikombe, kijiko na kontena) kwa kuzingatia rangi zilizoelekezwa zifuatazo:

Na.	TAHASUSI/COMBINATION	RANGI
1.	PCB	Nyekundu (Red)
2.	PCM	Bluu (Blue)
3.	CBG	Njano (yellow)
4.	CBA	Kijani (Green)
5.	HGL	Pinki (Pinc)
6.	HGK	Nyeupe (White)
7.	HKL	Blue bahari(Light blue

NB: Mwanafunzi aweke alama kwa kuandika jina lake katika vifaa hivyo, pia asisahau kopo la kuogea kulingana na rangi ya tahasusi/combination yake.

3.2.8 Tochi ya Betri au taa ya Sola kwa tahadhari umeme ukikatika

3.2.9 Madaftari makubwa (Counter Books) sita (6) au zaidi

3.2.10 Scientific Calculator kwa Wanafunzi wa Masomo ya Jiografia na Sayansi

3.2.11 Kitambulisho cha Bima ya afya (NHIF)

3.2.12 Nakala/kopi ya cheti cha kuzaliwa

3.2.13 Nakala/kopi ya hati ya matokeo ya kidato cha nne(statement of results).

3.2.14 Picha mbili (2) za passport size

3.2.15 Oxford advanced learners dictionary 1 na kamusi ya Kiswahili sanifu kwa masomo ya lugha

3.2.16 **VIFAA VYA USAFI**: Kila mwanafunzi alete vifaa vya usafi kama ilivyoainishwa hapo chini kulingana na Tahasusi:

1. **CBA:** Panga , jembe na kwanja
2. **PCB:**Chelewa ya kusimama, jembe na soft broom
3. **PCM:**Chelewa ya kusimama,jembe na hard broom
4. **CBG**:Chelewa ya kusimama , kwanja na soft broom
5. **HGL**: Jembe na mopper(Ndoo na dekio lake)
6. **HGK**: Chelewa ya kusimama, Reki na fagio la kutolea buibui
7. **HKL**: Rubber sqeezer na Mopper(ndoo na dekio lake).

NB: Kila mwanafunzi anapaswa kuleta vifaa vya usafi vilivyoainishwa na sio fedha taslimu. Vifaa vyote vitakaguliwa wakati mwanafunzi anaposajliwa.

4.0 MENGINEYO

4.1 Ni jukumu la mzazi/mlezi kumpatia mwanafunzi fedha kwa ajili ya matumizi binafsi awapo shuleni pamoja na kugharamia usafiri wa kuja shuleni na kurudi nyumbani wakati wa likizo. Fedha hizi apewe mwanafunzi mkononi, mzazi akadirie vema matumizi ya mwanae ili asiwe mbadhirifu au mdokozi.

4.2 Ni jukumu la mzazi/mlezi kuhakikisha afya bora ya mwanae kwa kumpatia matibabu stahiki kabla ya kuja shuleni. Mwanafunzi mwenye maradhi ya kudumu aje na barua ya uthibitisho kutoka kwa daktari wa hospitali ya Wilaya, Mkoa au Rufaa. Aidha mwanafunzi apatiwe fedha za matibabu kwa dharura itakayojitokeza.

4.3 Mwanafunzi awe na vifaa vya usafi binafsi kama vile doti moja ya kitenge (asije na kanga), taulo, mswaki, sabuni, mafuta ya kupakaa n.k(manukato hayaruhusiwi)

4.4 Ni mategemeo yangu makubwa kwamba Mwanafunzi atasoma kwa bidii, atatoa ushirikiano kwa wenzake kwa Walimu na Watumishi wengine na atazitii kanuni na sheria za shule katika kipindi chote awapo shuleni ili kuleta ufanisi na maendeleo ya shule.

4.5 Kila mwanafunzi aandike jina lake katika sare zake zote za shule pamoja na vifaa vyake vyote binafsi ili kuepuka kuchangia ua kupotea

4.6 Kabla ya kuripoti shuleni hakikisha umejaza fomu zifuatazo na uje nazo:

i. Fomu ya taarifa ya Mwanafunzi ya kukubali kujiunga na Shule.(Ijazwe na Mwanafunzi na kuthibitishwa na Mzazi)

ii. Fomu ya uchunguzi wa afya(Medical examination form)

4.7 Mzazi/Mlezi: Mawasiliano yote yamhusuyo mwanao yafanyike kupitia namba za simu zilizo katika Fomu hii. Epuka mawasiliano na mtu mwingine asiejulikana ili usitapeliwe. Usitume pesa kwa Mtu yoyote atakayekupigia bila kupata uthibitisho toka Shuleni. Mwisho hatupokei Mwanafunzi Siku za Jumamosi, Jumapili, sikukuu na Usiku(kwa sababu za kiusalama)

MWANAFUNZI ASIJE NA SIMU YA MKONONI KWANI HAZIRUHUSIWI SHULENI NA WALA HAKUNA SEHEMU YA KUZIHIFADHI. AIDHA MWANAFUNZI HARUHUSIWI KUSUKA NYWELE.

TAFADHALI SOMA KWA MAKINI MAELEKEZO/ MAAGIZO HAYA NA KUYATEKELEZA KIKAMILIFU.

Karibu sana Ruvu Sekondari
"Elimu ni Ukombozi"

CHIMAZI,J C
MKUU WA SHULE

TAARIFA ZA MWANAFUNZI.

1. Jina kamili la mwanafunzi kama lilivyotumika katika mtihani wa kidato cha nne

   ……

2. Tarehe ya kuzaliwa mwanafunzi. Tarehe……Mwezi…….Mwaka…….
3. Mahali alipozaliwa mwanafunzi

   i. Kijiji……

   ii. Wilaya…….

   iii. Mkoa……..

4. Kabila la mwanafunzi……..

5. Jinsia ya mwanafunzi……

6. Dini yake……

7. Jina la baba yake……

   Nambari yake ya simu……..

8. Jina la mama yake…….

   Nambari yake ya simu……..

9. Kama analelewa na mlezi, Jina kamili……

   Uhusiano na mwanafunzi……

   Nambari yake ya simu……

10. Shule ya Sekondari alikotoka mwanafunzi……..

11. Jina la mwenyekiti wa serikali ya mtaa……..
    Nambari yake ya simu……

12. Je ana magonjwa sugu? Kama ndio taja……..
    Anatibiwa hospitali gani……

Jina mzazi Sahihi

…….. ……

Tarehe……

HALMASHAURI YA WILAYA KIBAHA.
SHULE YA SEKONDARI RUVU

(ANUANI YA MZAZI)

……

……

YAH: **HATI YA KUKUBALI MASHARTI KUHUSU MTOTO WANGU KUSOMA SHULE YA SEKONDARI RUVU.**

Mimi……(Jina la Mzazi/Mlezi wa mwanafunzi) wa …….....

……(Jina la mwanafunzi)
Aliyekuwa akisoma Shule ya ……..(Taja jina la Shule aliyosoma

mwanafunzi) katika Wilaya ya …….Mkoa wa ……. Ninakubali mtoto wangu asome katika Shule ya Sekondari Ruvu iliyoko katika mji wa Mlandizi kwa kuzingatia masharti yafuatayo:

1. Kwamba mtoto wangu atahudhuria masomo kama kawaida na kufanya shughuli nyingine zote za Shule akikaa Shuleni kwa kipindi chote cha miaka miwili ya kidato cha tano na cha sita.
2. Kwamba kwa muda wote huo wa miaka miwili sitamsumbua Mkuu wa Shule, Afisa Elimu Sekondari Wilaya na Mkoa kuomba uhamisho.

Sahihi ya mzazi **Tarehe**

…… ……..

AHADI YA MWANAFUNZI.

Mimi……Nimekubali nafasi niliyopewa katika Shule ya Sekondari Ruvu. Ninaahidi kuwa mtiifu na kufuata kikamilifu **SHERIA, KANUNI** na **TARATIBU** halali zilizopo, pia ninaahidi kufanya bidii na kushirikiana na uongozi wa Shule na wanafunzi wenzangu katika kuendeleza taaluma na shughuli nyingine nitazopangiwa.

Jina la mwanafunzi **Sahihi**

…….. …….

Tarehe…….

SHULE YA SEKONDARY RUVU
FORM YA UCHUNGUZI WA AFYA
(REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION)

This form is to be complete by Medical Officer

Name of Student:……Age…….Sex……

The above named student has been examined in respect of:

I. STOOL……

II. URINE……..

III. PREGINANCY……..

IV. CHEST……

V. BLOOD……

VI. EYESIGHT……..

VII. HEARRING……..

VIII. HEART……..

IX. T.B……..

X. STOMACH ULCERS…….

XI. COMMENTS

……..
……

Name of Medical Officer……..Designation…….

Station……..Signature and Stamp……..Date……

1.**0 SHERIA ZA SHULE**.

Katika jamii yoyote ile ni lazima kuwepo na **SHERIA**, **KANUNI** na **TARATIBU** zitazowezesha jamii hiyo kuishi kwa kufuata maadili mema na mazuri ili kufikia malengo yanayotarajiwa.

1.**1 MAHUDHURIO**

i. Wanafunzi wote ni lazima wasome, waielewe na waifuate kwa makini ratiba ya kila siku.
ii. Kwakuwa lengo ni kupata elimu, wanafunzi wote lazima wahudhurie na kuwahi vipindi vya darasani, vipindi vya elimu ya kujitegemea, michezo na shughuli nyingine zozote za shule kama zitakavyopangwa katika ratiba ya shule isipokuwa kama ruhusa ya kutokuwepo itatolewa.
iii. Iwapo mwanafunzi atakosa shule kwa sababu yoyote ile ni lazima siku inayofuata aje na taarifa ya maandishi kutoka kwa mzazi/ mlezi au daktari kuelezea sababu za msingi zilizomfanya asihudhulie shuleni siku hiyo/hizo.
iv. Endapo mwanafunzi hatahudhuria shuleni kwa siku thelathini mfululizo bila taarifa yoyote atasimamishwa masomo na atafukuzwa shule kwa kutohudhuria siku tisini.
v. Mwanafunzi anaweza kufukuzwa shule kwa kosa la kukimbia/kutokuhudhuria na kutokufanya mitihani.
vi. Mwanafunzi hatoruhusiwa kutoka nje ya mazingira ya shule bila kibali maalum kitakachotolewa na mwalimu wa nidhamu/ darasa/zamu.
vii. Wanafunzi wote wanatakiwa kufuata ratiba ya siku kwa usahihi, kuanzia saa 11:30 alfajili hadi saa 04:30 usiku
viii. Wanafunzi wote watatakiwa kushiriki shughuli zote baada ya ratiba ya darasani kama elimu ya kujitegamea, clubs, debates, michezo na usafi wa mazingira.

1.2 **TABIA NA MWENENDO**.

Kuvunja miiko ifuatayo kunaweza kusababisha mwanafunzi kupata adhabu kali, kusimamishwa masomo au kufukuzwa shule kabisa:

i. Utoro
ii. Uzururaji
iii. Uasherati
iv. Wizi na uongo
v. Uvutaji bangi au ulevi wa aina yoyote ile.
vi. Utumiaji wa madawa ya kulevya.
vii. Kuchezea, kuharibu au kudharau alama za Taifa kama Bendera na waimbo wa Taifa.
viii. Kupigana au kutukana.
ix. Kutoa lugha ya matusi kwa yoyote yule.
x. Kugomea masomo, adhabu na maagizo yoyote yanayotolewa na walimu.
xi. Fujo na uchochezi usio na msingi unaoweza kuharibu amani.
xii. Kutofanya mitihani au mazoezi kwa makusudi na bila taarifa maalum.
xiii. Kuficha maovu, wahalifu na uhalifu.
xiv. Makosa ya jinai
xv. Kutoa mimba
xvi. Kupata mimba ndani ya shule

xvii. Kuolewa

xviii. Kutumia vibaya mali ya umma na hivyo kusababisha uharibifu na hasara.

xix. Kutoka nje ya mipaka ya shule bila kibali cha mwalimu anayehusika na malezi ya wanafunzi.

xx. Mwanafunzi haruhusiwi kuwa na simu ya mkononi, mawasiliano na mzazi yatafanywa kupitia makamu mkuu wa shule au mwalimu mlezi ataelekezwa kwao.Mwanafunzi atakegundulika kumiliki simu au vifaa vinaendana na simu kama line, battery, au handset atachukuliwa hatua za kinidhamu.

1.3 **HESHIMA**

i. Wanafunzi wote wanatakiwa kutii kengele.

ii. Wanafunzi wote wanatakiwa kuvaa sare ya shule kwa unadhifu, usahihi na kuchomekea wakati wote wanapokuwa katika sare ya shule. **ATAKAEVAA SKETI FUPI ITAKATWA NA KUTEKETEZWA ILI KULINDA HESHIMA NA MAADILI YA TAIFA**. Tunasisitiza heshima katika mavazi.

iii. Wanafunzi wote wanatakiwa kusimama parede kwa unadhifu na ukakamavu.

iv. Wanafunzi wasimame kusalimia walimu au mgeni aingiapo darasani.

v. Wanafunzi wasitoke darasani bila ruhusa na kwa makundi makundi.

vi. Wanafunzi wasipige kelele madarasani.

vii. Wanafunzi waheshimiane wao kwa wao na wawaheshimu viongozi wao.

viii. Hairuhusiwi kuzomeana darasani au nje ya darasa isipokuwakwa ruhusa ya mwalimu tu.

ix. Wanafunzi wawasalimie walimu au watu waliowazidi umri.

x. Wanafunzi wawaheshimu wafanyakazi wengine waliopo shuleni pamoja na maeneo ya jirani yanayozunguka shule.

xi. Wanafunzi wawe mfano bora katika fani zote heshima, kazi na usafi hata wanapokuwa nje ya mazingira ya shule.

1.4 MAVAZI

i. Wanafunzi wote watavaa sketi za rangi ya green(kijani) mshono wa linda boksi, shati nyeupe mikono mifupi pamoja na tai ya green yenye michirizi myeupe wakati wa saa za darasani. Wanafunzi washone sketi mbili za darasani zinazovuka usawa wa magoti.

ii. Pia kutakuwa na mavazi maalumu yanayovaliwa baada ya saa za masomo na sio mavazi ya nyumbani. Wanafunzi wanapawsa kushona sketi mbili za rangi ya dark bluu mavazi haya yatavaliwa na t-shirt ambazo zinapatikana shuleni. Mavazi ya nyumbani hayaruhusiwi.

iii. Kofia, viatu vya ghorofa(high heels) na mapambo mengine haviruhusiwi

iv. Wanafunzi wote wanatakiwa wawe na nywele fupi nadhifu. Hairuhusiwi kusuka nywele.

v. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na kucha fupi za mikono na miguu. Rangi ya kucha hairuhusiwi.

vi. Mwanafunzi atakaekwenda kinyume na mavazi rasmi yalioidhinishwa atanyang'anywa na hatarejeshewa.

vii. Wanafunzi wote watavaa viatu vyeusi vya ngozi na soksi nyeupe zisizo na marembo.

viii. Hijabu kwa Waislamu rangi nyeupe kwa wenye kulihitaji vazi hilo.

ix. Vifaa vya michezo track suit rangi ya bluu, jezi rangi ya bluu na jozi moja ya raba nyeupe.
x. Shuka nne rangi ya pinki, foronya na chandarua nyeupe ya pembe nne(square)
xi. Track suit moja ya rangi ya bluu kwa ajili ya masomo ya jioni(evening preparation) pamoja na soksi.

1.5 UTUNZAJI MALI.

i. Wanafunzi watatumia vizuri mali na vyombo vya umma kama vitabu, madawati, meza, viti na majengo kwa ujumla. Nimarufuku kuandika chochote katika mali hizo.Atakaekiuka na kujulikana adhabu kali itachukiliwa dhidi yake.
ii. Wanafunzi wanajukumu la kutunza mali yao mwenyewe na ile waliokabidhiwa kwa matumizi yao wawapo shuleni.
iii. Wanafunzi wote wanatakiwa kurejesha vifaa vyote vya shule kama vitabu na vinginenevyo kila wakati shule inapofungwa kwa mapumziko.
iv. Ni marufuku kuhamisha kifaa chochote kinachoweza kuhamishika kutoka mahali pake pa matumizi yaliodhinishwa. Endapo vifaa vitahamishwa kwenye vyumba vya madarasa kwa ajili ya kujisomea virejeshwe kwenye vyumba husika bila kuchanganywa kuepuka usumbufu.
NB: **UPOTEVU AU UHARIBIFU WA KIFAA CHOCHOTE CHA SHULE UTALIPWA NA MHUSIKA KWA GHARAMA HALISI ZA KIFAA HICHO**.

2.0 MIPAKA YA SHULE.

- Wanafunzi hawaruhusiwi kutoka nje ya mipaka bila kibali maalum.
- Wanafunzi hawaruhusiwi kufika sehemu zifuatazo:
  - Vilabu vyote vya pombe
  - Majumba ya starehe
  - Majumba ya kufikia wageni.
- Mwanafunzi atakaegundulika katoka maeneo ya shule bila kibali maalum atakuchuliwa hatua.

3.0 CHAKULA

Chakula cha wanafunzi kitapatikana shuleni. Hakutakuwa na chakula maalum. Wanafunzi wote watakula chakula kilichoidhinishwa.

4.0 MATIBABU

Wanafunzi walio katika utaratibu wa bima ya afya wataruhusiwa kutumia vitambulisho vyao vya Bima ya Afya.

Wasio na Bima ya Afya wataandikishwa katika utaratibu wa CHF kwa kulipia Sh. 5000 kila Mmoja.

5.0 MABADILIKO YA MAJINA NA ANUANI

- Endapo jina na anuani ya mzazi/mlezi vitabadilishwa kwa sababu yoyote taarifa itolewe shuleni ili rekodi za shule ziwe sahihi wakati wote na hasa wakati wa kupokea taarifa mbalimbali kwa wazazi/walezi kuhusu maendeleo ya mwanafunzi.
- Majina yaliyopokelewa shuleni ndio yatakayotumika bila kubadilishwa.
- Jina la mwanafunzi linaweza kubadilishwa endapo tu shule itapokea hati maalum kuhusu kubadilisha jina (hati ya mahakama).

VAZI LA DARASANI



VAZI LA KUSHINDIA (SHAMBA DRESS)

KOTI LA MAABARA KWA WANAFUNZI WA MASOMO YA SAYANSI

SWETA YA SHULE